# *September*

## *Inafaa kuwa tumaini letu kwamba matendo yetu yaishi zaidi ya mng'ang'ano wetu wa maisha*

Watu wa Mungu tunao soma kuwahusu katika agano la kale, waliishi muda mrefu sana. Musa kwa mfano, alifariki akiwa na miaka 120. Ibrahimu alikuwa miaka 175, na Nuhu aliishi hadi akafikia miaka 950! Inaonekana walikuwa na wakati wa kutosha kujifundisha kutokana na makosa yao na waache mfano wa kuishi maisha kwa njia ya Mungu. Lakini,bila kijalisha ni miaka ngapi ya ziada walipata, Bibilia hutueleza maisha ya mwanadamu ni mafupi sana yakilinganishwa na umilele.

Tuna muda kidogo sana wa kufanya jambo linalojalisha kwa anjili ya ufalme wa Mungu. Hata watu wenye Uungu hung'ang'ana. Yesu alielewa jinsi gani maisha hapa duniani yanaweza kuwa magumu. Haijalishi ni vizuizi gani inabidi tushinde, inafaa kuwa ni tumaini letu kwamba matendo yetu yazidi mng'ang'ano wetu wa dunia. Ni nini unaweza kufanya leo kuchangia 'picha kubwa' ya umilele wa Mungu?

*Ombi la leo*
Bwana, nisaidie nigundue muda wangu unawekewa kiwango, na kila dakika inaumuhimu. Ninataka kuishi maisha ambayo ni ya kupendeza Kwako; nionyeshe ni hatua zipi ninahitaji nichukue. Ahasante kwa kujalishwa na hata mambo madogo katika maisha yangu.

*Maandiko ya leo*

Yakobo 4:14Ninyi hamjui hata maisha yenu yatakavyokuwa kesho! Ninyi ni kama ukungu unaotokea kwa muda mfupi tu na kutoweka tena.

Luka Mtakatifu 21:33; Mbingu na dunia vitapita, lakini maneno yangu hayatapita.

## *Kuna dhibitisho kubwa ndani ya Neno inayounga mkono kupiga Kura kuliko ile ya kuinua mikono...*

Asili ya mwanadamu aliyeanguka ni kutamani kiwango cha kuelekeza ama kupigia kura kubainisha mambo yanayowahusu. Hata hivyo, ndani

ya Neno,  Mungu husimamisha mamlaka na kuchagua ni nani Atakayemuelekeza kwetu maishani. Maandiko yanatuonyesha wakati wowote Mungu hutuunganisha na mtu yeyote mmoja kwa jukumu moja, kila wakati Yeye huchagua mtu ambaye atasimamia. Hii ni kweli kwa jamii, kwa mtumwa na mkubwa wake, kwa ndoa, serikali, na kwa kanisa. Ukweli na mapenzi ya Mungu ni nadra, kama itakuweko, ikibainishwa na kuinua mikono. Ilionekana kwamba kila wakati wana wa Isiraeli walichagua kiongozi wao wenyewe kwa njia yao, ilimalizikia kwa janga. Labda hii ndio sababu Mungu anaweka mtindo wa kupiga kura ambayo ni kidogo zaidi ya kucheza karata, baada ya maombi mengi na kujitakasisha maisha yetu kwa Mungu. bila Neno wazi kutoka kwa Mungu, jambo lingine bora zaidi, katika hali nyingi, itakuwa ni kuamini kwa uteuwa kuliko yule amepewa kura nyingi. Hatutupilii mbali kutiwa moyo na washauri wa Uungu, lakini ni mmoja pekee anayeweza kuongoza na jina Lake ni Yesu. Muweke katika kiti chako cha dereva.

*Ombi la leo*
Mpenzi Baba, nionyeshe njia Zako na uelekeze maisha yangu kupitia Roho Wako Mtakatifu. Ninakuamini Wewe kuliko watu wengi. Nipee washahuri wa Neno Lako. Nikichagua na kuelekeza maisha yangu kupitia uingiliaji wa kiungu.

*Maandiko ya leo*
Waamuzi 6:40; Mungu akafanya hivi usiku ule, maan ile ngozi tu ilikuwa kavu, Napo palikuwa na umande juu ya nchi yote.

Matendo ya mitume 1:26Hapo, wakapiga kura; kura ikampata Mathia, naye akaongezwa katika idadi ya wale mitume wengine kumi na mmoja.

Yoshua 18:10 kisha Yoshua akapiga kura kwa ajili yao hapo mbele za Bwana katika Shilo; huko Yoshua akawagawanyia wana wa Iisraeli hiyo nchi sawasawa na mafungu yao.

Yona 1:7 wakasemezana kila mtu na mwenzake, haya, na mpige kura , mpate kujua mabaya haya yametupata kwa sababu ya nani.

## ***Usiruhu wanasiasa wachukue nafasi ya manabii.***

Hebu tuwazie Mungu alimwambia mchungaji wa kanisa ambaye anajulikana kwa wazi kama baba wa kanisa, anayeajibika kwa anjili ya maono, kwamba kanisa lafaa kutoa dola elfu kumi kama za kusaidia umeshanari wa inchi za mbali. Ni kawaida kwamba Mchungaji angeshiriki haya na uongozi wake wa chini na atafute ushauri wao wa maombi na kukubaliana kwao. Wazia kwamba wakati wa ushauri, viongozi wengine waanze kuulizana kuhusu kiasi cha pesa na wamuulize

mchungaji kurudisha kiwango chini hadi ibaki elfu moja. Mambo yanavyoendelea, hao viongozi, na labda hata mchungaji anaweza kujikuta akipanua mviringo wake wa watu wa ndani na aanze kitu ambacho ni kama kampeni ya kisiasa kutafuta watu wakumuunga mkono katika msimamo wake. Utaratibu wa siasa mara nyingi humalizikia kwa kutengana ama kukubaliana. Kama kanisa litamalizia kwa kutuma kiasi cha elfu tano pekee, basi hakuna yeyote atakayekuwa na hata nafasi kidogo ya kumtii Mungu. Tunapokubaliana na unabii ama turuhusu utaratibu wa siasa, kubadilisha maagizo ya Mungu, hakuna yule aliye na nafasi ya kupata ushindi. Aidha Mungu alisema toa elfu kumi, ama alisema usitoe chochote. Unabii waweza kuamuliwa lakini sio kwa utaratibu wa kisiasa. Siasa hukubaliana.

_Ombi la leo_
Mpenzi Bwana, ninaombea kanisa Lako. Weka siasa na hizo taratibu ambazo huelekeza kwa kukubaliana, mbali na kanisa. Nachagua kutobebwa ama kuingiana na wale wanaojaribu kunifanya nisimame upande wao. Nena kwa wazi na viongozi Wako walioteuliwa katika maisha yangu na nitafuata muongozo Wako.

_Maandiko ya leo_

Ufunuo 22:19 Na mtu yeyote akipunguza chochote katika maneno ya unabii yaliyomo katika kitabu hiki, Mungu atamnyang`anya sehemu yake katika ule mti wa uzima, na sehemu yake katika mji mtakatifu, ambavyo vimeelezwa katika kitabu hiki.

1 Wakorinitho 14:29 Kuhusu wale wenye kipaji cha kutangaza ujumbe wa Mungu, waseme wawili au watatu, na wengine wayapime maneno yao.

1 Samueli 15:24; ndipo Sauli akamwambia Samweli, Nimefanya dhambi maana nimeiharifu amri ya BWANA, pia na maneno yako; kwa sababu niliwaogopa wale watu, nikatii sauti yako.

## ***Kutii ni bora kuliko dhabihu***

Kuna kanuni tunayoielewa kutoka kwa Neno la Mungu inayotueleza kuwa hatuwezi kupata tena kwa dhabihu kile tulipoteza kwa kutotii kwetu. Hii ni kweli sio kwa mwanadamu pekee mbali hata na Mungu. ingawa Mungu alitoa dhabihu ya Mwanaye wa kiume kuokoa nafsi za wanadamu wote… sio wanadamu wote watakao okolewa. Mungu atapoteza nafsi zingine kupitia kwa kutotii kwa mwandamu ambazo hazitaweza kurejeshwa hata kupitia dhabihu ya mwanakandoo asiye na mawaa, Yesu, Masihi. Wote manabii Samuel na Isaya walinena ukweli

huu kwa uwazi. Isaya aliuliza swali, “mbona unatoa dhabihu? Sio kwa sababu umefanya dhambi?” aliendelea kusema kwamba Mungu anachukia dhabihu na alizihesabu kama uvundo katika mapua Yake kwa sababu inamkumbusha tu kuhusu dhambi za mwanadamu. Suruhisho, Isaya alisema, ni kuwacha kutenda uovu na kujifundisha kufanya mapenzi ya Mungu.

*Ombi la leo*
Mpenzi Baba, ahsante kwa kutoa dhabihu ya Mwanao Yesu kwa anjili ya dhambi zangu na kukubali malipo Yake kwa nafsi yangu. Sasa nisaidie nisitafuta dhabihu zaidi ninapowacha kutenda maovu na kujifunza kutenda wema.

*Maandiko ya leo*
Isaya 1:11; huu wingi wa sadaka senu mnazonitolea una faida gani? asema Bwana. Nimejaa mauta ya kafara za kondoo waume, na mafuta ya wanyama walionona; nami siifurahii damu ya ng’ombe wala ya wana-kondoo wala ya mbuzi waume.

Isaya 1:19-20 kama mkikubali na kutii mtakula mema ya nchi; mbali kama mkikataa na kuasi mtaangamizwa kwa upanga ; maana kinywa cha Bwana kimenena haya.

1 Samueli 15:22-23; naye Samweli akasema, Je! Bwana huzipenda sadaka za kuteketezwa na dhabihu sawasawa na kutii sauti ya Bwana.

## *Mungu anawatu pande zote mbili za mambo mengi*

Wakati wa vita za pili za dunia, inasemekana kwamba wanajeshi wa Ujerumani walikuwa Wakristo wakumaanisha na walikuwa na Bibilia zao kwa vilima wakitazama ufuoni wa bahari wa Normandy ilhali jeshi la kiAmerikani, ambao baadhi yao walikuwa Wakristo wenye kubeba Bibilia, walikuwa wakienda kuvamia ufuoni wa bahari hiyo ambayo ilikuwa imesimamiwa na Wajerumani waliojihami. Hata nimesikia ushuhuda wa kibinafasi kwamba kwa tukio limoja, ofisa wa Ujerumani, alipoana kikosi kilichokuwa kikiwajia, aliwaagiza wanajeshi wake wapige magoti, wainamishe vichwa vyao, na waombe ombi la Bwana mara moja ingine kabla wajipange. Wakati mwingine ni vigumu hata kuwazia kwamba Mungu aweza kuwa na watu pande zote mbili ambao wanaomba kwa dhati ili ufalme Wake uje na mapenzi Yake yatendeke wakiwa wanasimama na imani kwamba upande wao uko sawa. Labda hii ndio sababu moja Mungu anatuhimiza kupenda maadui wetu na tuwalishe wakiwa na njaa, kuwabariki tunapohisi kama waliotudhihaki, na tusiwahi kuchukua utukufu wa kibinafsi katika ushindi wetu badala yake wacha kulipishiwa kwote kuwe Kwake na Kwake pekee. Kuna

mambo yoyote katika jamii yako ama taifa ambayo yanaweza kuwa na waumini pande zote mbili?

*Ombi la leo*

Mpenzi Mungu, nisaidie niwe na huruma kwa watu wengine hata wakati labda hawajaamini kama mimi ama hawatazami mambo kwa mtazamo wangu. Nifundishe kuwachukulia wengine kwa njia ambayo ningetaka kuchukuliwa hata mimi, kwa jina la Yesu.

*Maandiko ya leo*

Warumi 14; 1-7; Mkaribisheni kwenu mtu aliye dhaifu, lakini msibishane naye juu ya mawazo yake binafsi. Watu huhitilafiana: mmoja imani yake inamruhusu kula kila kitu; lakini mwingine ambaye imani yake ni dhaifu, hula tu mboga za majani. Mtu ambaye hula kila kitu asimdharau yule ambaye hawezi kula kila kitu; naye ambaye hula tu mboga za majani asimhukumu anayekula kila kitu, maana Mungu amemkubali. Wewe ni nani hata uthubutu kumhukumu mtumishi wa mwingine? Akisimama au akianguka ni shauri la Bwana wake; naam, atasimama imara, maana Bwana anaweza kumsimamisha. Mtu anaweza kufikiria siku fulani kuwa ya maana zaidi kuliko nyingine; mtu mwingine aweza kuzifikiria siku zote kuwa sawa. Kila mmoja na afuate msimamo wa akili yake. Anayeadhimisha siku fulani anaadhimisha siku hiyo kwa ajili ya kumtukuza Mungu; naye anayekula chakula fulani anafanya hivyo kwa kumtukuza Bwana maana anamshukuru Mungu. Kadhalika naye anayeacha kula chakula fulani anafanya hivyo kwa ajili ya kumtukuza Bwana, naye pia anamshukuru Mungu. Maana hakuna mtu yeyote miongoni mwetu aishiye kwa ajili yake mwenyewe, wala hakuna anayekufa kwa ajili yake mwenyewe

## *Kama unataka kuwa kama Yesu, lazima uende kanisani*

Kanisa ni mwili wa Krsito, Bibi harusi wa Kristo, na jamii ya Mungu duniani. Waefeso inatuambia lwamba Yesu alikufa kwa anjili ya kanisa, Mwili Wake, na Bibi Harusi Wake. Ni mapenzi ya Mungu kwamba kila muumnini afanyike  kiungo kinachofanya kazi cha jamii ya wanaoamini. Hata hivyo, watu wengi hawawazii kuwa wanao wakati wakufanya uamuzi kama huo. Badala ya kuwa umeokoka na kuwa na agano na Bibi arusi wa Kristo, wanatenda kazi ni kama kwamba wao ni wachumba wa kike wa Yesu. Wanaweza kukosa kugundu ani kiwango gani analipenda kanisa na jinsi gani amajitoa kwa ajili yake. Katika Agano la Kale, Mungu aliwalea wana Wake kuhudhulia kanisani kwa kuwaamuru wajitoe , wahudhulie dhabihu, na walete sadaka na zaka zao. Yesu pia alikuwa na tabia ya kuhudhulia kanisa. Hapa ndipo aliendа shule,

alijifunza kusoma, alihubiri mara ya kwanza, na alipokuwa wakati wa Sabato. Kuongeza kwa hayo, picha ya mbinguni na shughuli zake za kuabudu mwana kondoo wa Mungu ni kama picha ya ibada ya kanisani. Ikiwa utaenda mbinguni, utaenda kanisani! Pendeza Mungu na ujitolee maisha yako kwa kanisa la karibu.

*Ombi la leo*

Baba, nataka kukushukuru Kwa sababu ya jamii uliumba kwa ajili yetu hapa duniani. Najitoa mwenyewe kuwa sehemu ya kanisa langu la nyumbani pahali utakaponiweka. Nifanye mwenye mazao na unipe neema, katika jina la Yesu

*Maandiko ya leo*

Waebrania 10:25: Tusiache ile desturi ya kukutana pamoja, kama vile wengine wanavyofanya. Bali tunapaswa kusaidiana kwani, kama mwonavyo, Siku ile ya Bwana inakaribia.

Luka Mtakatifu 4:16: Basi, Yesu alikwenda Nazareti, mahali alipolelewa, na siku ya Sabato, aliingia katika sunagogi, kama ilivyokuwa desturi yake. Akasimama ili asome Maandiko Matakatifu kwa sauti.

Malaki 3:10 leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu, mkanijaribu kwanjia hiyo; asema Bwana wa majeshi mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni , na kuwamwagieni baraka, hata isikuweko nafasi ya kutosha, au la.

## ***Wakufunzi wa darasa la kwanza sio wapumbavu***

Sio kumaanisha wakufunzi wa darasa la kwanza hawaelewi mahesabu ya Calculus; lakini ni kuwa wana ufahamu wa kutojaribu kufundisha calculus kwa wanafunzi wa darasa la kwanza. Pengo kuu katika wakufunzi na wanafunzi, inaletwa ujuzi unaopatikana katika msemo wa kimithali -darasa la kwanza. Kutoka hapa kuendelea, pengo huenda likipunguka hadi siku moja mwalimu anagundua huyu mwanafunzi amemzidi kwa maarifa, hekima, ama ujuzi. Hata hivyo haijalishi mtu atapanda ngazi ya maisha, hatimaye, hawatapata usalama kuliko msingi wao.

Kwa sababu hii, lazima tusiwahi kuchoshwa na kuweka msingi imara kwa maisha ya wale tunaogusa kwa sabau za Kifalme. Usidharau wakati ambao umetumika vizuri kwa kujifunza kanuni za Ukristiano ambazo ni rahisi na za msingi.

*Ombi la leo*

Ewe Bwana, nifundishe kutosheka na urahisi wa Neno Lako na kutowacha upendo wangu wa kwanza. Nisaidie kuweka msingi wa maisha yangu juu ya Mwamba ambao ni Kristo.

*Maandiko ya leo*

Mathayo Mtakatifu 7: 24-27; "Kwa sababu hiyo, kila mtu anayeyasikia maneno yangu na kuyazingatia, anafanana na mtu mwenye busara, aliyejenga nyumba yake juu ya mwambaMvua ikanyesha, mito ikafurika, pepo kali zikavuma na kuipiga nyumba hiyo. Lakini haikuanguka kwa sababu ilikuwa imejengwa juu ya mwamba. "Lakini yeyote anayesikia maneno yangu haya bila kuyazingatia, anafanana na mtu mpumbavu aliyejenga nyumba yake juu ya mchanga. Mvua ikanyesha, mito ikafurika, pepo kali zikavuma na kuipiga nyumba hiyo, nayo ikaanguka; tena kwa kishindo kikubwa."

2 Wakorinitho 11:3Lakini naogopa kwamba, Kama vile yule nyoka kwa hila zake za uongo alimdanganya Hawa, fikira zenu zaweza kupotoshwa, mkauacha uaminifu wenu wa kweli kwa Kristo.

## ***Jambo moja utakalojutia ukufika mbinguni ni kwamba haukuenda awali***

Bibilia inaeleza Mungu aliumba mbinguni ya kupendeza hivi kwamba hatuwezi kufikiria itakuwa nzuri kiasi gani. hebu jaribu kuwazia ni nzuri kiasi gani…mapito ya dhahabu, hakuna uchungu, hakuna machozi, hakuna dhambi, na hakuna kushindwa. Hauchoki wala haupati njaa, hewa ni ya kupendeza. Kila kitu huko kinapendeza. Unaweza kufikiria? La, hauwezi. Mungu alisema itakuwa bora kuliko mawazo yako.

Niamini, asilimia mia moja ya kila mtu ambaye ameenda mbele yetu wako vizuri kutuliko sisi, na kama unaweza wauliza waamue kurudi baada ya kuingilia lango za lulu, wanaweza kutaka kukaa huko. Wakati utavuta pumzi yako ya mwisho hapa duniani, utaweza kusema kwa ujasiri kwamba siku yako kuu iko mbele bado.

*Ombi la leo*

Ahsante Mungu, kwa sababu ya usoni wa kupendeza kiasi hicho. Ninafurahishwa na umilele. Baba, Neno Lako huniambia kuwa nijibidiishe na upanuzi wa ufalme hadi utakapokuja. Najitoa kufanya yote niwezayo kujenga milki Yako duniani. Nionyeshe jinsi ya kufanyika

mfanyi kazi bora. Naomba kwamba nitaacha mambo tunayoweza kuongea kuhusu huko mbinguni.

*Maandiko ya leo*

1 Wakorinitho 2:9Lakini, ni kama yasemavyo Maandiko Matakatifu: "Mambo ambayo jicho halijapata kuyaona wala sikio kuyasikia, mambo ambayo binadamu hajapata kuyafikiria moyoni, hayo ndiyo Mungu aliyowatayarishia wale wampendao."

1 Petero1:4na hivyo tunatazamia kupata baraka zile ambazo Mungu aliwawekea watu wake. Mungu amewawekeeni baraka hizo mbinguni ambako haziwezi kuoza au kuharibika au kufifia.

Ufunuo 14:13; Kisha nikasikia sauti kutoka mbinguni ikisema, "Andika! Heri watu ambao tangu sasa wanakufa wakiwa wameungana na Bwana." Naye Roho asema, "Naam! Watapumzika kutoka taabu zao; maana matunda ya jasho lao yatawafuata."

## ***Hatufanyi kazi ili tumalize ila ili tufanye kazi nzuri***

Hatufai kusema kazi imefanyika hadi ifanyike vyema. Kwa sababu sio lengo letu kukamilisha pekee ila kukamilisha vizuri. Wakati mwingine msukumo wa kumaliza hufunika utaratibu hadi tunapoteza uhalisi wa matokeo yetu. Hii ni kweli sio kwa usimamizi na uundaji pekee, lakini hata katika nyanja za kiroho za maisha. Hali za kiroho za maombi,sifa, masomo ya Bibilia, na masomo ya hiari yaweza kwa wakati mwingine, kufanyika kama utaratibu wa kila siku na wakati mwingine hata jambo la kuchokesha tunapojikuta tukipitia juu pekee ili tumalize na tuweke alama kwamba hiyo tumefanya na tuendelee kwa jambo litakalofuatia. Jitie moyo siku ya leo kuangalia kwa makini kazi uliyoko nayo na umalize jambo moja vyema kabla kuendelea kwa lingine. Utajikuta ukiwa umetosheka zaidi, una mazao mwengi zaidi, na ukiwa umebaki na muda mwingi zaidi hatimaye.

*Ombi la leo*

Mpenzi Mungu, nisaidie niangalie kwa umakini mambo ambayo ninahusika, hasa yale ya kiroho. Naungama kukupa mawazo yangu na sio tu wakati wangu. Nisaidie nimalize kazi Yako ambayo umenipa nifanye kama nimekimbia mbio yangu na kumaliza sehemu yangu vyema.

*Maandiko ya leo*

Waefeso 5:16…Tumieni vizuri muda mlio nao maana siku hizi ni mbaya.

Kumbukumbu la Torati 6:5; nawe mpende Bwana, Mungu Wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote.

2 Timotheo 4:7; Nimefanya bidii katika mashindano, nimemaliza safari yote na imani nimeitunza.

## ***Msamaha ni haki, urejesho ni jukumu***

Yesu alipopeana maisha Yake msalabani kalivari, alitununua kutoka kwa dhambi na tukapewa upenyo wa msamaha. Msamaha, ukitaka ni haki. Hata wakati tunashusha wengine moyo, wanaamuliwa watusamehe. Kuongezea, Bibilia inatuambia kwamba tukikiri dhambi zetu kwa Mungu, yeye ni mwaminifu kutusamehea dhambi zetu, hapo akituahidi msamaha kwa wale wanaouliza. Tunaposamehea mtu, ambayo ni haki yao, inamaanisha hatutamani tena kuwaona wakiadhibiwa kwa sababu ya kosa lao. Tunaacha kufuata kujilipishia, kulipwa, ama tunawachana na kuona tumekosewa. Msamaha ni haki, hata hivyo urejesho ni jukumu. Waweza kusamehea mtu ama usamehewe na mtu bila uhusiano kurejeshwa kabisa. Urejesho mara nyingi hugharimu pande iliyokosea ikitubu na kufanya jitihada zinazotoka kwa roho za maridhiano. Chunguza uhusiano wako. Umesamehewa? Umerejeshwa? Utafanya nini kuhusu jambo hili?

*<u>Ombi la leo</u>*

Baba wa mbinguni, nipe neema na nguvu kusamehea wengine wanaponikosea na unisaidie kuchukua kila hatua inayofaa kurejeshwa na wengine ninapoleta kosa na kusimama nikihitaji kusamehewa mwenyewe. Amina.

*<u>Maandiko ya leo</u>*

I Yohana 1:9 Lakini tukiziungama dhambi zetu, basi Mungu ni mwaminifu na mwadilifu, naye atatusamehe dhambi zetu na kututakasa na uovu wote.

Luka Mtakatifu 6:37"Msiwahukumu wengine, nanyi hamtahukumiwa; msiwalaumu wengine, nanyi hamtalaumiwa; wasameheni wengine, nanyi mtasamehewa.

2 Wakorinitho 5:20 Basi, sisi tunamwakilisha Kristo, naye Mungu mwenyewe anatutumia sisi kuwasihi ninyi. Tunawaombeni kwa niaba ya Kristo, mpatanishwe na Mungu.

Zaburi 133:1; Tazama, ni vizuri na inapendeza wakati wa ndugu wanaishi pamoja kwa umoja.

## *Ifanye iwe rahisi, iseme mara nyingi, ifanye iteketee*

Kielelekezo cha kuwa mwana habari aliyefaulu, ni kufanya ujumbe uwe rahisi, urudie mara nyingi, na uhakikishe umewasilishwa kwa kutaka. Sisi tumeitwa ili tuupitishe ujumbe wa Yesu Kristo kwa njia inayoaminika na kukumbatika. Tunapomwambia mtu kuhusu injili ya Yesu Kristo ama tunaposhiriki kanuni za maisha kutoka kwa Neno la Mungu, mtu tunayemwambia anafaa kuwa na uwezo wa kurudia ujumbe huu kwa mtu mwingine. Kwa hivyo ni ya muhimu kuangalia kwa umakini mambo ambayo Mungu anatupatia sisi kusema na tunayapange kwa njia ambayo yatafikia alama yake, yatimize malengo ya Mungu, na yafikie matokeo makubwa kama inavyowezekana. Hii inamaana kuwa ni lazima tuangalie kwa makini ukweli tunaoshikilia kama wa maana sana na tuuweke kwa njia ambayo wale watakaosikia wataweza kukumbuka na kurudia ukweli huu kwa wengine.

*Ombi la leo*

Mpenzi Bwana, tafadhali nisaidie niwe mpitishaji wa ujumbe wa Injili anayefaulu na ninapokomaa kuelewa kwamba matokeo ya ujumbe ni muhimu kama ujumbe wenyewe. Nisaidie kunena kwa njia ambayo wanaonisikiliza watapokea ninachosema na wabebe ujumbe kwa watu wengine.

*Maandiko ya leo*

2 Wakorinitho 11:13Maana, hao ni mitume wa uongo, wafanyakazi wadanganyifu wanojisingizia kuwa mitume wa Kristo.

Kumbukumbu la Torati 6:7-9 nawe wafundishe watoto wako kwa bidii na kuyanena uketipo katika nyumba yako na utembeapo njiani na ulalapo na uondokapo. Yafunge yawe dalili juu ya mkono wako nayo yatakuwa kama utepe katikati ya macho yako. Tena yaandike juu ya miimo ya nyumba yako na juu ya malango yako.

2 Timotheo 2:2Chukua yale mafundisho uliyonisikia nikitangaza mbele ya mashahidi wengi, uyakabidhi kwa watu wanaoaminika, ambao wataweza kuwafundisha wengine pia.

## *Kama haikuchomi ndani, haitawachoma ndani wanao kusikiliza*

Katika maisha yetu, tunasikia mazungumuzo yasio ya maana sana, kutoka kwa hadithi, mazungumuzo, mahubiri, mazungumzo ya baada ya taarifa, na mazungumzo yasiyokuwa na maana kutoka kwa jamii na marafiki. Maneno ambayo hayana manda hayamaanishwi kugusa hisia Fulani. Mazungumuzo yasiyo na maana ni mengi sana  kwamba wakati mwingi watu huchukulia kutoka kwa wanaonena na kuendelea na mazungumuzo yenye maana kidogo katika ubongo wao na mawazo yao. Hii ni kwa sababu mambo muhimu maishani hushikwa, sio kufundishwa. Upashaji habari mkuu ambao hata historia inakumbuka, yote ilikuwa na jambo limoja kwa usawa. Upendo wa ujumbe wa wakati wao. Iwe ni amri jeshi mkuu, viongozi wa dunia, washairi, ama wana sarakasi wakiwa jukuani, shauku lao liliamuru kusikizwa kwa makini na wasikilizaji wao na pia ikalazimisha uamuzi wao. Kaa na sahuku yako nayo itakaa na wengine.

*Ombi la leo*

Baba, nipe upendo na ufanye upia kukubali kwangu kwa ukweli ulio kwa Neno Lako. Koroga Roho yangu ili ninene kwa ujasiri, nikiwa na ushujaa, na niwasilishe tamaa ichomayo ya Mapenzi Yako, katika jina la Yesu. Amina.

*Maandiko ya leo*

Waebrania 10:35 Basi, msipoteze uhodari wenu, maana utawapatieni tuzo kubwa.

Luka Mtakatifu 4:36Watu wote wakashangaa, wakawa wanaambiana, "Hili ni jambo la ajabu, maana kwa uwezo na nguvu anawaamuru pepo wachafu watoke, nao wanatoka!"

Mathayo Mtakatifu 12:36; "Basi, nawaambieni, Siku ya hukumu watu watapaswa kujibu juu ya kila neno lisilofaa wanalosema.

## *Mambo muhimu maishani Yanashikwa sio kufundishwa*

Jinsi watu hufundishwa imegawanishwa kwa viwango hivi vipana: wale wanaojifunza kwa kusikiliza, wale wanaojifundisha kwa kutenda, na wale wanaojifunza kwa kusoma. Ukweli, tunaelewa kuwa watu wengi wanamchanganyiko wala hawajifunzi kwa njia moja pekee. Kwa upana,

mafunzo mengi ya maisha hupatikana kutoka kwa mojawapo ya njia hizi za elimu.hata hivyo, mambo muhimu maishani, yanashikwa mara nyingi sio kufundishwa. Mambo muhimu ninayosema i yanashirikisha mambo ya roho wa Mungu ambayo ni ya ndani na yasiokamatika kama vile maneno matupu yanaweza kuwasilisha ama kupitisha. Kwa sababu hii sote sisi tunaojifunza na wanaofundisha kanuni za Kifalme lazima wamiliki upako unaotokana na upako wa Roho Mtakatifu, ambaye Yeye binafsi ni ukweli mwingi, uletao ufunuo, uhuisho, na motisha kwa roho za waume kwa wake kwa dakika. Omba kwamba Mungu akupe na wale wanaokufunza upako unaohitajika kudhihirisha mambo muhimu ya ukweli wa maisha.

*Ombi la leo*

Mungu nipe mimi na wakufunzi wangu upako wa Roho Mtakatifu ili tuweze kubainisha kwa usawa Neno Lako la Ukweli.

*Maandiko ya leo*

1 Yohana 2:27 Lakini, kwa upande wenu ninyi, Kristo aliwamiminieni Roho wake. Na kama akiendelea kukaa ndani yenu, hamhitaji kufundishwa na mtu yeyote. Maana Roho wake anawafundisheni kila kitu na mafundisho yake ni ya kweli, si ya uongo. Basi shikeni mafundisho ya huyo Roho na kubaki katika muungano na Kristo.

## *Upinzani hauna faida...utapotelea kwa wingi*

Mungu anampango, atafaulu, na, kwa sasa, una fursa ya kushiriki. Hata hivyo kushiriki katika mpango wa Mungu kwa wanadamu wote ni jambo la uamuzi kwa kila muumini. Mungu anataka dunia yote isikie Habari Njema na wakubali Yesu kuwa Bwana na Mwokozi. Anataka uende uwaambie wengine kuhusu mpango Wake kwa maisha yao, na ni lipi kuhusu mpango wa Mungu kwa maisha yako? Ni mapenzi ya Mungu yenye uamuzi kufanya kazi ndani yako juu yako akitarajia kufanya kazi kupitia kwako, na hata kama hautawahi chagua kufanyika shahidi wa Kristo, Mungu ameamua kukufanyia kazi bila kujalisha hayo. Mungu hatakoma kufanya kazi juu ya maisha ya kila muumini hadi kila mmoja akuwe mkamilifu na awe kama mfano wa Mwanaye mpendwa, Yesu. Mungu amekata kauli hata kama itagharimu atumie umilele wote! Kwa nini tusifanye kazi na Yeye kwa vile upinzani wako hauna faida na unarefusha utaratibu?

*Ombi la leo*

Mpenzi, Bwana, nionyeshe jinsi ninaweza kufanya kazi na Wewe unapofanya kazi ndani yangu na juu yangu ili ufanye bora zaidi kupitia kwangu. Sitapingana na nguvu za roho mtakatifu ambazo zinanibadilisha mimi.

*Maandiko ya leo*

Warumi 8:29 Maana hao aliowachagua tangu mwanzo, ndio aliowateua wapate kufanana na Mwanae, ili Mwana awe wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi.

1 Yohana 3:2 Wapenzi wangu, sisi ni watoto wa Mungu sasa, lakini bado haijaonekana wazi jinsi tutakavyokuwa. Lakini tunajua kwamba wakati Kristo atakapotokea, tutafanana naye kwani tutamwona vile alivyo.

2 Wakorinitho 3:18; Basi, sisi sote ambao nyuso zetu hazikufunikwa, twaonyesha kama katika kioo, utukufu wa Bwana; tunabadilishwa tufanane zaidi na huo mfano wake kwa utukufu mwingi zaidi. Hiyo ni kazi yake Roho wa Bwana.

## *Ni lengo letu kwamba mazao yetu yastahimili utaratibu wa uundaji*

Mungu ameunda maisha kwamba kila kitu kizae "kulingana na mfano wake". Hadithi ya uumbaji kutoka kwa kitabu cha Mwanzo inatengeneza mfano wa maisha yote. Mungu alipoumba miti, mimea, samaki na bahari, ndege wa angani, wanyama wa mbugani, na hata mwanadamu, aliamuru kwamba kila maisha yawe na mbegu ndani yake itakayozaa ingine mfano wake. Sheria inaweza kupanuliwa na kujengwa juu yake kulingana na maandiko kushirirkisha mambo mengi zaidi ya maisha. Uwekezaji wa kila siku wa mbegu ya urafiki, kama tu vile mbegu mbaya huharibu tabia nzuri za watu ambao kwa kawaida ni watu wazuri. Kwa sababu hii, tunafaa kutazama kwa karibu mambo yale yanayotuzunguka na tunenee maisha yetu. Kwa mfano, kama tunatamani kufaulu, kuwa na mazao, furaha, ama watakatifu tunafaa kutafuta kuingiana na wale wanothihirisha mambo haya. Na, usisahau, maisha sio kukuhusu wewe pekee, wekeza kwa wengine.

*Ombi la leo*

Baba wa mbinguni, nipe uhusiano unotamani kwa maisha yangu ili niweze kujifundisha kutokana na wengine na niweze kuwafundisha wale walio na hitaji. Nitenganishe na wale wanaoweza kunielekeza kwa ubaya na kunifanya nisitii neno Lako.

*Maandiko ya leo*

1 Wakorinitho 15:33 Msidanganyike! Urafiki mbaya huharibu tabia njema.

Mithali 18:24 ajifanyaiye rafiki wengi ni kwa uangamivu wake mwenyewe; Lakini yuko rafiki aambatanaye na mtu kuliko ndugu.

Mwanzo 1:11 Mungu akasema, Nchi na itoe majani, mche utoao mbegu , na mti wa matunda uzaao matunda kwa jinsi yake, ambao mbegu zake zimo ndani yake, juu ya nchi; ikawa hivyo.

## *Ongoza ukiwa na maono*

Kwa wakati Fulani maishani kila mtu hujikuta akiwa pahali pa uongozi, akiketi kwa kiti cha ndereva, akibainisha ni njia gani tunageukia. Hii ni kweli hata kama unajiongoza mwenyewe tu kupitia maishani. Kabla mtu yeyote kufanya uamuzi bora zaidi kuhusu upande atakao kugeukia, lazima kwanza waelewe ni wapi wanapoelekea. Uongozi huamuru mambo mengi kwa mtu mmoja, lakini hakuna lililo likuu kama kuwa na ujasiri na upande wanakoelekea. Kwa sababu hii, ni muhimu kujua mambo mawili ya maisha; Kwanza lazima tujue tuko wapi kwa ramani ya maisha na la pili tunahitaji kuwa wapi. Kwa wakati wowote, bila kujalisha kugadamika, misukumo tunayokutana nayo, tunaweza kusimama na kuchora mstari ulionyooka kutoka pale tulipo sasa hadi kwa Mungu na hii utatupea mwelekeo wazi. Usiende mbali tena bila kuwa na ujasiri kwamba hatua yako inayofuata itakuelekeza karibu na mpango wa Mungu kuhusu maisha yako. Ongoza ukiwa na maono!

*Ombi la leo*

Baba, ninaomba kwamba unipe maono Yako kuhusu maisha yangu na uyafanye yawe wazi ili niweze kuwa na mwelekeo dhabiti na nisiyumbayumbe njiani za ulimwengu huu. Nisaidie kujiongoza mwenyewe na wengine kuelekea mapenzi Yako.

*Maandiko ya leo*

Mithali 29:18 pasipo maono, watu huacha kujizuia; bali ana heri mtu yule aishikaye sheria.

Matendo ya Mitume 16:9-10 Usiku huo, Paulo aliona ono ambalo alimwona mtu mmoja wa Makedonia amesimama pale na kumwomba: "Vuka, uje Makedonia ukatusaidie." Mara baada ya Paulo kuona ono

Hilo, tulijitayarisha kwenda Makedonia bila kukawia, tukiwa na hakika kwamba Mungu ametuita tuwapelekee Habari Njema.

Habakuku 2:2 Bwana akanijibu akasema, iandike njozi ukaifanye iwe wazi sana katika vibao, ili aisomaye apate kuisoma kama maji.

## *Usiwahi kupuuza nguvu za mtazamo halisi maishani*

Kuna msemo wa zamani unaosema, " bila kujalisha kama unaona unaweza ama unaona kama hauwezi, labda uko sahihi." Maisha ni namna hii. Kwa nini? Kwa sababu ameamuru maisha yaweze kukupa jawabu, kulingana na jinsi unavyowaza, unavyonena, na vile unaamini. Maisha yangu yote, nimegundua kwamba watu wenye mtazamo wa ushindi, wanauwezo mkubwa maishani kuliko wale wenye mtazamo wa kushindwa. Mtazamo wa kushindwa sanasana husababisha mfadhaiko na kuhisi kama hakuna usalama. Ilhali watu huazima shida na kuwazia mabaya sana, wanabaki wakiishi kwa uoga, wakihofia na kufadhaika kuhusu mambo mengi ambayo hayafanyiki. Kwa upande wingine, wale walio na mtazamo wa usawa, san asana huwa na raha, amani, na subira hata ndani ya matatizo. Unaamini nini?  Unakiri ni nini na unaendelea namna gani maishani?

*Ombi la leo*

Bwana, nitafanya niwezayo yote, nitaamini mazuri iwezekanavyo, na ninene mazuri kuhusu siku zangu za usoni na pia za wengine. Nisaidie katika jina la Yesu,Amina. -

*Maandiko ya leo*

Wafilipi 4;8 hatimaye ndugu zandu, mambo yo yote yaliyo ya kweli, yo yote yaliyo ya staha,  yoyote yaliyo ya haki, yoyote yaliyo safi, yo yote yenye kupendeza, yo yote yenye sifa njema, ukiwapo wema wowote, ikiwamo sifa nzuri yoyote, yatafakarini hayo.

Mithali 18:21; mauti na uzima huwa katika uwezo wa ulimi; na wao waupendao watakul amatunda yake.

Mithali 6:2; basi umetengwa kwa maneno ya kinywa chako, umekamatwa kwa maneo ya kinywa chako.

## *Unaweza kuanza historia yako siku ya leo*

Kabla mtume Paulo apate mwito wake wa kubadilishwa katika barabara ya Damesiki, alijulikana vyema kama mtu anayewatesa wale walioamini kwamba Yesu ni masihi. Hiyo siku ilibadilisha maisha yake na akaanza historia mpya. Kila mmoja wetu anafursa sawa ya kuanza sura mpya ya maisha katika pahali popote tunapochagua. Katika kila uamuzi tunaoufanya, tuna andika hadithi ambayo wengine watasoma kutuhusu. Anza shani mpya leo ukiwazia jinsi unataka historia ikukumbuke. Fanya amuzi zitakazo thibitisha tabia na namna ya maisha unayotamani na kwa kila uamuzi, ongeza sura kwa historia ya maisha yako.

*Ombi la leo*

Baba wa mbinguni, nachagua kujenga jinsi watu wananijua karibu na Neno Lako. Niasaidie kufanya kila uamuzi uandamane na tabia ya muumini katika Yesu. Nikianguka, tafadhali nisamehe, niinue juu, na uniruhusu kuanza tena. Naamua kusahau ya kale na kukumbatia ya sasa ninapong'ang'ana kuelekea kwa alama ya mwito mkuu Ulionao kwa sababu yangu katika Kristo.

*Maandiko ya leo*

Mithali 22:1 heri kuchagua jina njema kuliko mali nyingi; na neema kuliko fedha na dhahabu.

Wafilipi 3:13 ndugu, sijidhanii nafsi yangu kwamba nimekwisha kushika; ila natenda neno moja tu; nikiyasahau yaliyo nyuma; nikiyachuchumilia yaliyo mbele.

Isaya 43:18-19 msiyakumbuke mambo ya kwanza, wala msiyatafakari mambo ya zamani. Tazama ninatenda neno jipya; sasa litachipuka. Je! Hamtalijua sasa? Nitafanya njia hata jangwani, na mito ya maji nyikani.

## ***Pahali palipo mtaji wakushiriki, lazima pawe pia, kwa sababu ya haja, majukumu yanayoshirikianwa.***

Miaka kadhaa iliyopita kanisa letu lilinunua jengo kwa sababu ya kanisa tulilokuwa tumeanza Urusi. Liko katika maili 500 kaskazini mashariki mwa Moscow, majira ya hewa ya baridi yaweza kuwa mabaya sana ikiwa na upepo kutoka kaskazini na kuleta theruji katika pahali ambapo baridi ni ya kugandamiza. Jengo hili mpya lilikuwa na mtambo wa kupasha njoto kupitia kuchoma mafuta. Mafuta yalikuja kupitia kwa mfereji kutoka kwa debe ambalo pia liliyapa majengo yaliyoko karibu

mafuta pia. Ingawa mitaji hii tulioshiriki na wengine ilitusaidia, na bila hii waumini hawangemiliki hili jengo, halikuwa huru. Kama mtu anavyoweza kufikiria, mitaji hii ya kushirikiana ilikuja na jukumu pia la kushirikiana kulipa kwa mafuta tuliyotumia na gharama ya kuhifadhi mtambo huu. Hivi ndivyo ilivyo kwa kila mtu anayepokea manufaa kutoka kwa ufalme wa Mungu na/ ama na kanisa la nyumbani…kila mmoja anashiriki kwa jukumu la kusaidia kulipa wafanyikazi, kusimamisha kazi ya Mungu, kuona kwamba nafsi zetu zimeokolewa kwa neema yake ya utwalia. Unafanya kazi yako?

*Ombi la leo*

Mungu, nataka kutenda sehemu yangu. Ahsante kwa kumtuma Yesu kuokoa nafsi yangu na pia kwa kuwatuma wengine kwa njia yangu kunifundisha na kushiriki maisha na mimi. Nisaidie kuwa mtu mwenye kujukumika anayefanya sehemu yake katika jina la Yesu.

*Maandiko ya leo*

2 Wakorinitho8:11-15; Basi, kamilisheni shughuli hiyo; na kama vile mlivyokuwa na hamu kubwa ya kusaidia, basi, fanyeni bidii vivyo hivyo, kadiri ya uwezo wenu, kuikamilisha. Maana Ninyi hampaswi kuongezewa taabu kusudi wengine wapunguziwe mzigo wao; sivyo, ila ni lazima tujali usawa na haki. Kila mlicho nacho sasa cha ziada kiwasaidie wale wanaohitaji, ili nao wakati watakapokuwa na ziada, wawasaidie ninyi katika mahitaji yenu, na hivyo kuwe na usawa. Kama Maandiko yasemavyo: "Aliyekusanya kwa wingi hakuwa na ziada, na yule aliyekusanya kidogo hakupungukiwa."

## *Mkristo ni nini?*

Utajauaje kama mtu ni mkristo? Ni kwa sababu wanafuata imani, tamaduni, na mafunzo ya kanisa lililo na mpangilio, iwe ni Katoliki, Baptisti, Assembly of God, Presbyterian, Lutheran, Greek orthodox, Armenian, ama kikundi cha dini zinazoingiana? Labda watu wengine husema wana shina la Ukristo kutokana na kurithi kutoka kwa mababu, mila, tamaduni, desturi ama urithi wa kikabila. Hata hivyo, ukweli ni kwamba 'Ukristo' inamaanisha kuwa kama Kristo…kuwa mfuasi wa Yesu. Bibilia inasema kuwa waumini waliitwa Wakristo Antioki, miaka mingi baada ya kifo cha Yesu na baada ya kanisa la kwanza kuzaliwa. Kunaonekana hapa kuwa na mtindo Fulani ambao unagharimu umakini wetu. Kabla kuitwa Mkristo, watu kwanza walitambuliwa kama waumini wa Yesu kama Masihi, Kristo aliyeteuliwa. Hivyo ndivyo ilivyo siku ya leo na itakuwa hivyo milele. Mkristo sio Mkristo kwa sababu amezaliwa katika jamii ya Wakristo, ameiga tamaduni ama desturi Fulani, anafuata

jadi Fulani, ama amejiunga na kanisa Fulani. Ili mtu afanyika mfuasi wa Yesu, lazima kwanza afanyike muumini. Hii inagharimu uamuzi wa kibinafsi na wa ukweli ambao kisha unagharimu kuungama imani yetu kwamba sisi ni Wake. Wewe ni Mkristo?

*Ombi la leo*

Mpenzi Bwana, naamini kwamba Yesu wa Nazarethi ni mwana Wako na Mwokozi wangu. Ninamkubali kama Bwana wangu na nitachagua kila siku kufuata Neno Lake kama kawaida ya maisha yangu. Naomba kwamba wengine waweze kumwona Kristo ndani yangu.

*Maandiko ya leo*

Matendo ya Mitume 11:26 -Alipompata, alimleta Antiokia. Nao wote wawili walikaa na lile kanisa kwa mwaka wote mzima wakifundisha kundi kubwa la watu. Huko Antiokia, ndiko, kwa mara ya kwanza, wafuasi waliitwa Wakristo. ic

Warumi 10:9-10 -Kama ukikiri kwa kinywa chako kwamba Yesu ni Bwana na kuamini moyoni mwako kwamba Mungu alimfufua kutoka wafu, utaokoka. Maana tunaamini kwa moyo na kukubaliwa kuwa waadilifu; na tunakiri kwa midomo yetu na kuokolewa.

## *Ni lazima niwe Myahudi ili nifanyike Mkristo?*

Hili swali lilijadilianwa kati ya mitume kwa kanisa la kwanza Yerusalemu. Matendo ya mitume 15, inaelezea kuhusu mazungumzo na uamuzi wa Yakobo, mchungaji wa kanisa na ndugu wa kambo wa Yesu. Iliamuliwa hakuna anayehitaji kubadilika afanyike Muyuda ili awe muumini wa Yesu kama Masihi. Hatusikii tena swali hili, lakini tunakutana na maswali mengi ya namna hii katika maisha yetu. Dini nyingi za kanisa linagharimu kwamba mtu abadilishwe kwa imani yao na ukawaida wao kabla akubalike kama muumini wa kweli aliye na haki kwa manufaa ya Ufalme wa Mungu. hii, rafiki yangu sio ukweli, na haifai kukumbatiwa kama sharti la wakovu. Hata hivyo, ukizaliwa mara ya pili, ni ya kueleweka kwamba tuabudu na kushirikiana na waumini wengine ambao wanaushawishi kama wetu, kuhusu imani,kanuni, na ukawaida. Ruhusu Mungu akuweka ndani ya kanisa kama inavyompendeza Yeye na sio kama inavyompendeza mwanadamu, ilhali ukimpa kila muumini mwingine heshima na haki sawa.

*Ombi la leo*

Baba, nisaidie kukumbuka kwamba mimi kwanza ni muumini aliyejitoa Kwako na nimeitwa kutumika katika pahali pa mapenzi Yako kuhusu maisha yangu. Nisaidie kuwa na neema na hekima kukubali wengine ambao umeita ambao sio kama mimi kabisa. Nitenganishe na kuwa wa kuhukumu, kusengenya, ama kujitenga kwa maana umejumuisha kila mtu kwa mpango Wako.

*Maandiko ya leo*

Yohana 10:16 Tena ninao kondoo wengine ambao hawamo zizini humu. Inanibidi kuwaleta hao pia, nao wataisikia sauti yangu, na kutakuwako kundi moja na mchungaji mmoja.

Matendo ya Mitume 15:19-20 "Kwa hiyo, uamuzi wangu ni huu: tusiwataabishe watu wa mataifa wanomgeukia Mungu. Bali tuwapelekee barua kuwaambia wasile vyakula vilivyotiwa najisi kwa kutambikiwa sanamu za miungu; wajiepushe na uasherati; wasile mnyama yeyote aliyenyongwa, na wasinywe damu.

1 Wakorinitho 12:18 Lakini kama ilivyo, Mungu alizipanga sehemu hizo tofauti katika mwili kama alivyopenda

## *Maisha ni mtihani, pita kwa sababu, ni mtihani kutoka kwa kitabu kilicho wazi*

Hata majaribu magumu kabisa na majaribio ya maisha yamegusiwa katika Bibilia. Wakati mwingi tunahisi ni kama tunajaribiwa na hali na matukio tunayokumabana nayo. Maisha yaweza kuwa magumu wakati mwingine na baadhi yetu hatuna asili nzuri kufanya mitihani.

Habari Jema! Mitihani inayokuja kwa njia yetu inamajibu. Majibu haya yameandikwa kwa Neno la Mungu. Kila mtihani ni kutoka kwa kitabu kilicho wazi na pia tunahimizwa kuuliza maswali na kutafuta majibu kutoka kwa waalimu na kutoka kwa wengine wengi ambao wameshafanya mitihani hii. Usife moyo. Usipoupita mtihani wakati huu, sanasana, tutaufanya mara nyingine. Fungua Kitabu!

*Ombi la leo*

Baba, nagundua kutoka kwa Neno Lako kwamba Wewe hauwajaribu ama kuwatahini wana Wako kwa mabaya. Najua kwamba sio Wewe mwanzilishi wa uovu unaokuja kwa njia yangu…Wewe ni jawabu la shida zangu zote. Nifunze Neno Lako na unipe nafasi ya kuwasaidia wengine katika mitihani yao ya maisha. Ahsante kwa Bibilia.

*Maandiko ya leo*

2 Timotheo 3:16 Maandiko yote Matakatifu yameandikwa kwa uongozi wa Mungu, na yanafaa katika kufundishia ukweli, kuonya, kusahihisha makosa, na kuwaongoza watu waishi maisha adili,

Yakobo 1:13; Kama mtu akijaribiwa, asiseme: "Ninajaribiwa na Mungu." Maana Mungu hawezi kujaribiwa na uovu, wala yeye hamjaribu mtu yeyote.

## ***Sio lazima uwe kama mimi kufurahisha Yesu, lakini ni hakika kuwa itabidi uwe kama wewe.***

Mungu anakupenda sana kukuacha jinsi ulivyo. Hii ndio sababu amenihimiza kuandika hizi kanuni za imani ya maisha na kushiriki na wewe ambaye Yeye amenipea. Nagundua kwamba kwa kushiriki mambo mengi kuhusu maisha yangu na kuamini kwangu kibinafsi, inaweza kuonekana kama mimi ni mamlaka Fulani katika maisha ama uhisi ni kama kwamba watu wengine wanafaa kuwa zaidi kama mimi. Niamini, siwazii kama mimi ndiye mwenye majibu ya maswali yote, lakini najua ni nani Aliyenayo. Pia siamini kwamba ukifanyika zaidi kama mimi itatengeneza shida za kila mmoja wetu kuona kwamba hata mimi nina shida na ninakumbana na shida za kawaida za maisha. Sio lazima uwe kama mimi zaidi ili uwe kama Yesu, lakini itabidi uwe kama wewe. Kwa nini? Kwa sababu sisi wote humjia Bwana kama undongo kwa mikono ya mfinayanzi mkuu na Yeye hutuunda na kututengeneza kadri ya mapenzi Yake, akiumba ndani yetu uwezekano wa kumpendeza na kufanyika kama Yeye zaidi. Jiachilie kwa kazi ya Mtawala unapotazama zaidi ya imani hii kwa Yule ambaye kwa ukweli anakunenea. Sikia sauti ndani ya sauti na ukubali kubadilishwa siku ya leo.

*Ombi la leo*

Mpenzi Bwana, nataka kuwa kama Wewe zaidi na ninaomba msaada Wako. Nionyeshe mambo ambayo lazima yabadilike katika maisha yangu na unifanye kama undongo kwa mikono Yako.

*Maandiko ya leo*

Isaya 64:8 lakini sasa Ee Bwana, wewe u Baba yetu, sis tu undongo, nawe u mfinyanzi wetu; sisi sote tu kazi ya mikono yako.

Yeremiah 18:6 Ee nyumba ya Isiraeli,je! Siwezi mimi kuwatendea nyinyi vile vile kama mfinyanzi alivyotenda?  Asema Bwana. Angalieni, kama

undongo ulivyo katika mkono wa mfinyanzi ndivyo mlivyo ninyi katika mkono wangu, Ee nyumba ya Isiraeli.

## *Kufaulu kwa ufalme wa Mungu kunagharimu watu vikundi vinne: wanaoenda, wanaobaki, wanaomba, na wanaolipa.*

Jeshi hutumia mambo kadhaa ya umuhimu. Kwanza kuna wale wanaokubali na kujitolea kuenda kwa vita na kukumbana na maadui katika uwanja wa vita ambao hawajauzoea. Pili, kuna umuhimu kwa wale wanaojitolea kubaki nyuma, kulinda watu wa taifa na mali yao. Tatu ni wale ambao wamefunzwa kuweka laini za kupitisha ujumbe zikiwa sawa kati vikundi mbali mbali na amri jeshi mkuu. Hizi laini za kupitisha ujumbe ni muhimu ili kupokea maagizo , kuitisha vifaa muhimu, na kueleza ni nini kinacho endelea. Na wa mwisho lakini sio kumanisha ana umuhimu kidogo ni wale wanaonekana ni kama hawana kazi lakini bila hao jeshi halingekuweko. Hawa ni wananchi wanaoenda njia yao wakitengeneza pesa na kulipa ushuru ambazo hatimaye husaidia jeshi letu nyumbani na huko uwanjani. Ufalme wa Mungu na hata kanisa sio tofauti. Kwa kila moja kumaliza misheni yao inahitaji wanaoenda, wanaobaki, wanao omba, na wanaolipa. Kuko wapi kujitolea kwako na upendo wako? Mungu amekufanya kuwa kitu gani?

*Ombi la leo*

Mungu ninataka kuwa kiungo muhimu kwa Ufalme Wako na kanisa langu. Najua kwamba umeniumba na kusudi na umeniandaa kukutana na haja Fulani. Nionyeshe sehemu yangu na nitajitoa kufanya pahali pangu. Ahsante.

*Maandiko ya leo*

1 Wakorinitho 12:12, 14, 18, 19, 20 Kama vile mwili ulivyo mmoja wenye viungo vingi, na viungo hivyo vyote--ingawaje ni vingi--hufanya mwili mmoja, ndivyo ilivyo pia kwa Kristo. Mwili hauna kiungo kimoja tu, bali una viungo vingi. Lakini kama ilivyo, Mungu alizipanga sehemu hizo tofauti katika mwili kama alivyopenda. Kama sehemu zote zingekuwa kiungo kimoja, mwili ungekuwa wapi? Ukweli ni kwamba, sehemu za mwili ni nyingi, lakini mwili ni mmoja.

## *Msingi wa injili sio yale unayoweza kufanya nay ale hauwezi lakini ni ...imeshafanyika*

Msingi wa sheria ya Musa ulikuwa kuhusu masharti, maagizo ya maisha, yanayofaa kutendwa na yasiyofaa, ukitaka. Siku moja ungekubalika kwa Mungu na nyingine ukataliwe. Sheria inagharimu kanuni, hukumu, na adhabu. Chini ya sheria hakuna mwanadamu aliyekuwa na haki na wote walihukumiwa.

Vitabu vya Injili, hata hivyo, huonyesha picha tofauti. Wakati Mwana wa Mungu alipeana maisha Yake kulipia dhambi za wanadamu wote, mambo yalibadilika. Sheria ilitosheka, hukumu ikatumikiwa, na faini ikalipwa. Hatutafuti tena kumsongelea Mungu kupitia mambo yanayofaa kutendwa na yasiyofaa, lakini kupitia "imetendwa" iliyowekwa wakfu.Yesu alitenda, imetendeka, na sisi, kwa imani, tumefanyika waridhi wa kazi hiyo ambayo imekamilika. Hatuweki sheria za Mungu ili tuweze kukubalika na Yeye lakini tunafanya mapenzi Yake kwa sababu tumeshakubalika na Yeye.

*Ombi la leo*

Baba, namkubali mwanao Yesu kama Mwokozi wangu na namuweka kwa kiti cha enzi cha maisha yangu. Nachagua kuishi maisha yangu kwa imani katika kazi Yake ambayo imakamilika.

*Maandiko ya leo*

Warumi 3:20-22 hakuna binadamu yeyote anayekubaliwa kuwa mwadilifu mbele yake Mungu kwa kuishika Sheria; kazi ya Sheria ni kumwonyesha tu mtu kwamba ametenda dhambi. Lakini sasa, njia ya Mungu ya kuwakubali watu kuwa waadilifu imekwisha dhihirishwa, tena bila kutegemea Sheria. Sheria na manabii hushuhudia jambo hili. Mungu huwakubali watu kuwa waadilifu kwa njia ya imani yao kwa Yesu Kristo; Mungu hufanya hivyo kwa wote wanaoamini; hakuna ubaguzi wowote.

Wagalatia 2:20 na sasa naishi, lakini si mimi tena, bali Kristo anaishi ndani yangu. Maisha haya ninayoishi sasa naishi kwa imani, imani katika Mwana wa Mungu aliyenipenda hata akayatoa maisha yake kwa ajili yangu.

***Wakati mwingine mambo hayafanyiki kwa sababu hayatafanyika kwa mtu mwingine yeyote ila wewe***

Mara nyingi Mungu anaponena na wewe, ni kwa sababu anataka kufanya kazi kupitia kwako na kuwapa watu wengine kazi hiyo haitakamilisha kazi. Chukua hadithi ya Elisha na yule mwanamke Mshunami, katika Wafalme wa Pili 4. Mwana wake wa kiume alishikwa na ugonjwa na akafa kwa ghafla. Akaenda kwa manabii na kuwaambia matatizo yake. Akiwa na shaka nyingi, Elisha akawatuma wafanyi kazi wake katika mkono wa mtumishi wake uwekelewe juu ya mtoto na umfufue kutoka kwa wafu. Hata hivyo, wakati mtumishi wa Elisha aliporudi, alileta riporti kuwa huyo mtoto hakuwa na mabadiliko.

Wakati huu, Elisha akafanya safari mwenyewe na akawekelea mwili wake juu ya mwili wa yule mtoto, na Mungu hapo kwa hapo akafufua yule mtoto. Ni kwa nini muujiza huu ukakosa kufanyika kwa yule aliyetumwa na Elisha?  Sijui ni kwa nini, lakini ninajua kwamba; wakati mwingine mambo hukataa kufanyika kwa sababu hayatafanyika kwa mtu mwingine yeyote ila wewe.

*Ombi la leo*

Baba wa mbinguni, natamani Wewe Uninenee mimi na ufanye kazi kupitia kwangu kwa mkono wangu na wale ninaotuma kutenda kazi Yako. Nifundisha kujua ni miujiza gani lazima niwekelee mkono wangu na ni gani ninaweza kuwapa wengine. Ahsante Bwana, Amina.

*Maandiko ya leo*

2 Wafalme 4:31-35; Na Gehazi akawatangulia, akaiweka ile fimbo juu ya mtoto, lakini hapakuwa na sauti wala majibu. Basi, akarudi ili kumlaki akamwambia akisema, mtoto hakuamka. Basi Elisha alipofika nyumbani tazama, mtoto amekwisha kufa amelazwa kitadani pake. Basi akaingia ndani akajifungia mlango, yeye na yule mtoto, wote wawili, akamuomba Bwana. Akapanda juu ya kitanda akajilaza juu ya mtoto, akaweka kinywa chake juu ya kinywa chake, na macho yake juu ya macho yake, na mikono yake juu ya mikono yake akajinyosha juu yake; mwili wake yule mtoto ukaanza kupata moto. Kisha akarudi akatembea nyumbani, huko na huko mara moja; akapanda akajinyosha juu yake na yule mtoto akapiga chafya mara saba. Na mtoto akafumbua macho yake.

***Kama unataka kuwa Na siku za usoni Kama uotavyo, lazima uende kazini sasa kwa ajili ya siku za usoni.***

Alikuwa kitu kama mwanzilishi wa shida kwa karibu maisha yake yote. Ukweli mbinu yake ile ya hivi majuzi ilimalizika vibaya sana kwake kwamba alitoka nyumbani na tumaini kidogo sana ya kurudi. Kile alikuwa nacho tu ni jina la mtu wa ukoo wao wa mbali, akili zake, na uhusiano mpya na Bwna.

Kisha akakutana na Raheli. Na sasa, Yakobo alijua siku zake za usoni zilikuwa na nini, kwa maana alikutanana msichana wa ndoto zake. Hata hivyo kujua tu lengo ni gani haikumhakikishia kufaulu; Yakobo alifanya kazi ili ifanyike. Akafanya mpango na baba wa huyu msichana na akaanza kufanya kazi ili ajionyeshane kuwa wa ukweli na pia ili awe na hazina ya siku zake za usoni. Bwana alikuwa amempea Yakobo tumaini la siku njema ya kesho, lakini bado alimtarajia ashiriki Kwa huu mpango. Kupitia mambo haya, Yakobo alijufunza somo muhimu alilopitisha kwa mmoja wa wanawe. Huwezi kumsikia akimwambia mwanawe, mwenye ndoto, asife moyo wakati mambo yanakuwa magumu? “Kumbuka Yosefu kama utakuwa na siku za usoni kama ulivyo ota, lazima uende ufanye kazi sasa kwa ajili ya siku za usoni.”

Huo ni ushauri mzuri leo!

*<u>Ombi la leo</u>*

Baba, Neno Lako linasema kwamba unampango mzuri kwa maisha yangu, kunipa tumaini na siku za usoni! Ninapotazamia siku za usoni zinazoningojea, tafadhali noinyeshe mambo ninayohitaji kufanya sasa kufanya itimie. Ahsante Baba kwa kunipa nguvu kufanya kazi kwa bidii kwa sababu ya yale yako mbele zangu.

*<u>Maandiko ya leo</u>*

Mwanzo 29:18 – Yakobo akampenda Raheli, akasema nitakutumikia miaka saba kwa kumpata Raheli, binti yako mdogo

## ***Mtu huenda mbali na Mungu, wakati aidha, Mungu anasonga na hatusongi... ama tunapo ondoka tukielekea pahali Mungu hawezi***

Kutembea mbali na Mungu hakuonekani kama hakuna maana kwa wakati huo.  Wakati mmoja maishani, Ibarahimu na  mwana wa ndugu yake Lutu, waliona ilikuwa sawa watengane kwa sababu ya kuelewana. Walikuwa wamebarikiwa sana na Bwana kwamba wafanyi kazi wao walikuwa wameanza kugombana kuhusu mitaji. Abrahamu kwa upole, akampa Lutu uamuzi wa kwanza abako angewalisha mifugo yake. Hapa

sasa ndipo Lutu akafanya kosa kubwa. Bibilia hutuambia kwamba Lutu alichagua…' "yeye mwenyewe".

Hii inaweza kaa ni kama sio ya muhimu, lakini ukweli ni kwamba Lutu hakutafuta ushauri kutoka kwa Bwana kama mjomba wake alivyofanya. Yeye, kwa hakika, alitafuta arthi iliyo onekana bora zaidi. Lakini Mungu alifahamu kile Lutu hakufahamu- pahali alipokuwa akihamia hapakuwa na umilele. Bwana aliharibu mji huo ambao Lutu alikuwa kiongozi, na akapoteza kila kitu. Alijifunza kama amechelewa ya kwamba mtu husongea mbali na Mungu wakati, aidha Mungu alisonga na hatukusonga…ama tuliposonga kuelekea pahali Mungu hawezi. Kufaulu ni vizuri, lakini hakuna uzuri unaoweza kuonekana tunapochagua vibaya kama Lutu na kujiweka mbali na Mungu alipo. Hakikisha kila wakati unasongelea karibu na Mungu.

*Ombi la leo*

Bwana, nataka kukupendeza kwa yote ninayofanya, na kwa kila uamuzi ninaofanya. Tafadhali nipe masikio ya kusikia sauti Yako vizuri, macho yanayotafuta kazi Yako, na Roho inayokupenda kuliko mambo mengine yote. Ninaposoma Neno Lako tafadhali nionyeshe jinsi ya kufanya uamuzi mzuri. Nataka kukufuata Wewe- usiache nipotee!

*Maandiko ya leo*

Mwanzo 13:11; basi Lutu akajichagulia Bonde Lote la Yorodani; Lutu akasafiri kuenda upande wa mashariki; wakatengana wao kwa wao. Abrahamu akakaa katika nchi ya Kanaani, na Lutu akakaa katika miji ya lile Bonde; akajongeza hema yake mpaka Sodoma. Lakin watu wa Sodoma walikuwa wabaya, wenye kufanya dhambi nyingi sana juu ya Bwana.

## ***Huenda Mungu hawezi kulipia kile hakuagiza***

Wazia ukiwa kwa mkahawa na mtumishi akaanze kujaza meza yako na vyakula ambavyo haukuwa umeitisha. Bila kujalisha chakula cha onekana ni kizuri kiasi gani, kinaonja ama kunukia ni vigumu kwamba utalipa kwa sababu ya vitu hukuwa umeitisha. Utasikia je mtumishi yule yule akikulazimisha ulipie chakula kile chote?

Hii ilinifanyikia juzi katika nchi ya ugeni. Hata kama nilikuwa mpole, hata hivyo nilikuwa imara. Kwa mshangao wa mtumishi, nilikataa maombi yote na nika kataa kulipa kwa zile vitu sikuwa nimeagiza. Wakati mwingine, naamini Mungu hufanya hivyo hivyo. Yeye hana lazima kulipa kila gharama tunayojichukulia wenyewe. Kuwa na

maombi kabla uamue ni nini bora zaidi kwa Mungu na anafaa kutumia pesa zake wapi ama unaweza kukutana na kulipa hiyo gharama wewe mwenyewe.

*Ombi la leo*

Baba, ninenee na unipe hakima kujihusisha tu kwa mambo ambayo ninajua yako ndani ya mapenzi Yako. Nisaidie nisipoteze mitaji Yako kwa mambo ambayo Wewe hauwezi.

*Maandiko ya leo*

Luka Mtakatifu 12:16-20- Kisha akawaambia mfano: "Kulikuwa na tajiri mmoja ambaye shamba lake lilizaa mavuno mengi. Tajiri huyo akafikiri moyoni mwake: `Nitafanyaje nami sina mahali pa kuhifadhia mavuno yangu? Nitafanya hivi: nitabomoa ghala zangu na kujenga kubwa zaidi, na humo nitahifadhi mavuno yangu yote na mali yangu. Hapo nitaweza kuiambia roho yangu: sasa unayo akiba ya matumizi kwa miaka na miaka. Ponda mali, ule, unywe na kufurahi Lakini Mungu akamwambia: `Mpumbavu wewe; leo usiku roho yako itachukuliwa. Na vitu vile vyote ulivyojilundikia vitakuwa vya nani?"`

Yakobo 4:13-15 Basi, sasa sikilizeni ninyi mnaosema: "Leo au kesho tutakwenda katika mji fulani na kukaa huko mwaka mzima tukifanya biashara na kupata faida. Ninyi hamjui hata maisha yenu yatakavyokuwa kesho! Ninyi ni kama ukungu unaotokea kwa muda mfupi tu na kutoweka tena. Mngalipaswa kusema: "Bwana akitujalia tutaishi na tutafanya hiki au kile."

## ***Ni mtoto wako, wewe mlee***

Miaka kadhaa iliyopita mzee na mkewe walitembelea kanisa letu. Wakauliza nafasi na wakapata na mimi kushiriki yale maono waliyoamini Mungu aliwapa. Niliposikiliza nikawa na shauku kwamba walikuwa hawaelewi jambo muhimu sana kwa maono yoyote…kujukumika ili kushughulikia jambo baada ya kuzaliwa. Unaona, waliniambia wana mwito wakusaidia makanisa kwa kuanza huduma ya basi. Hata hivyo baada ya kuzungumza sana walibaki watu ambao hawajajitolea kufanya kwa hiyo huduma ama kujukumika kwa jambo lolote linalohusu kushughulikia na kufaulu. Walitamani kutunga mimba kanisa letu na mbegu yao ya kutamani lakini hawakusikia kama wanajukumu lakutoa chochote baadaye. Ukweli ni kwamba wao sio washirika wa kanisa lolote ama huduma ila yao wenyewe. Niliwakemea

kwa kukosa kina ama kufikiria makanisa ama viongozi wa makanisa, walikuwa hawana maono. Sio maono tunakosa lakini ni watu ambao wamejitolea kufanya kazi kwa huduma baada ya kuzaliwa. Kwa hivyo Mungu akikufanya baba ama mama wa huduma, jipeane kufanya zaidi ya kuzaa…lea mwana.

*Ombi la leo*

Mpenzi Bwana, nisaidie kuwa na hisia nzuri na kuajibika zaidi ya kuwatunga mimba tu watu wengine na mafikira yangu. Nipe hakima inayohitajika kuendelea kushughulikia zile vitu ambazo zitazaliwa kupitia kwangu.

*Maandiko ya leo*

2 Wakorinitho 11:28 Na, licha ya mengine mengi, kila siku nakabiliwa na shughuli za makanisa yote.

2 Wakorinitho 8:16 Namshukuru Mungu aliyeweka ndani ya moyo wa Tito hamu hiyo niliyo nayo mimi ya kuwasaidia.

Wafilipi 2:20 maana sina mtu mwingine mwenye nia moja nami; atakayeiangalia hali yenu kweli kweli.